

VIGEZO NA MASHARTI YA UANACHAMA

1. ORODHA YA STAHIKI ZA HUDUMA KWA KIFURUSHI CHA NAJALI AFYA

- i) Ada ya kujandikisha na kumwona daktari.
- ii) Huduma ya kulazwa hadi siku 30 kwa mwaka kwa kila mnufaika.
- iii) Dawa zote zinazoruhusiwa katika ngazi ya Zahanati na Kituo cha Afya kwa kuzingatia Mwongozo wa Matibabu Tanzania (STG).
- iv) Huduma za vipimo vya maabara na uchunguzi aina 162 tofauti vikiwemo X-RAY, ECHO, EEG, Ultrasound.
- v) Huduma za kuziba na kung'oa meno.
- vi) Huduma za matibabu ya macho.
- vii) Huduma za kujifungua zinatolewa baada ya kuchangia mfululizo katika kipindi cha miaka miwili (2).
- viii) Huduma za upasuaji mdogo aina (27) na upasuaji mkubwa aina (14)
- ix) Huduma za matibabu ya kibingwa hadi Hospitali ya Rufaa. Kwa Hospitali za Kanda, Taifa na Hospitali Maalum ni kwa kuzingatia taratibu za rufaa.

2. ORODHA YA STAHIKI ZA HUDUMA KWA KIFURUSHI CHA WEKEZA AFYA

- i) Ada ya kujandikisha na kumwona daktari.
- ii) Huduma ya kulazwa hadi siku 45 kwa mwaka kwa kila mnufaika mmoja.
- iii) Dawa zote zinazoruhusiwa katika ngazi ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya kwa kuzingatia Mwongozo wa Matibabu Tanzania (STG).
- iv) Huduma za vipimo vya maabara na uchunguzi aina 197 tofauti vikiwemo X-RAY, ECHO, EEG, Ultrasound. Kipimo cha CT Scan kinatolewa kuanzia mwaka wa pili wa uchangiaji.
- v) Huduma za kuziba na kung'oa meno.
- vi) Huduma za matibabu ya macho.
- vii) Huduma za kujifungua zinatolewa kuanzia mwaka wa pili wa uchangiaji.
- viii) Huduma za upasuaji mdogo aina 30 na upasuaji mkubwa aina 36
- ix) Huduma za matibabu ya kibingwa hadi Hospitali ya Rufaa. Kwa Hospitali za Kanda, Taifa na Hospitali Maalum ni kwa kuzingatia taratibu za rufaa.

3. ORODHA YA STAHIKI ZA HUDUMA KWA KIFURUSHI CHA TIMIZA AFYA

- i) Ada ya kujandikisha na kumwona daktari.
- ii) Huduma ya kulazwa hadi siku 60 kwa mwaka kwa kila mnufaika.
- iii) Dawa zote zinazoruhusiwa katika ngazi ya Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa za mikoa kwa kuzingatia Mwongozo wa Matibabu Tanzania (STG).
- iv) Huduma za vipimo vya maabara na uchunguzi aina 223 tofauti vikiwemo X-RAY, ECHO, EEG, Ultrasound. Vipimo vya CT Scan na MRI vinatolewa kuanzia mwaka wa pili wa uchangiaji.
- v) Huduma za kuziba na kung'oa meno.
- vi) Huduma za matibabu ya macho.
- vii) Huduma za kujifungua zinatolewa kuanzia mwaka wa pili wa uchangiaji.
- viii) Huduma za upasuaji mdogo aina 50 na upasuaji mkubwa aina 80
- ix) Huduma za matibabu ya kibingwa hadi Hospitali ya Rufaa. Kwa Hospitali za Kanda, Taifa na Hospitali Maalum ni kwa kuzingatia taratibu za rufaa.

KUMBUKA:

1. Uanachama ni kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura 395 TL 2015 na Kanuni zake za Mwaka 2002.
2. Huduma ambazo hazijaaishwa katika vifurushi husika hazitagharamiwa na Mfuko.
3. Huduma zitatolewa katika vituo vyote vilivyosajiliwa na Mfuko (Umma, Binafsi, na Madhehebu ya Dini) kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa. Huduma katika ngazi za Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Taifa zitatolewa kwa utaratibu wa rufaa.
4. Mwanachama anashauriwa kufanya maamuzi sahihi kabla ya kuamua kuchangia kifurushi anachokitaka. Kwani utaratibu huu hauruhusu kurejesha fedha mara baada ya malipo.
5. Kadi ya matibabu itaanza kutumika siku 30 baada ya tarehe ya malipo ya michango.
6. Mwanachama atapaswa kuhuisa uanachama wake ndani ya siku 30 tangu tarehe ya mwisho ya mchango wa awali. Vinginevyo vigezo vya mwanachama anayejingga kwa mara ya kwanza vitatumika".
7. Muda wa matumizi ya kadi ni mwaka mmoja. Matumizi ya kadi ya mchangiaji yatakoma sambamba na kadi zote za wategemezi wake.
8. Mfuko una haki ya kufanya mapitio ya mafao yake wakati wowote bila kulazimika kutoa taarifa za awali kwa wanachama.
9. Vigezo na masharti ya kifurushi husika kuzingatiwa.
10. Kwa maelezo na ufanuzi zaidi, tafadhalii wasiliana na ofisi ya NHIF iliyo karibu au piga namba 0800 110063 bila malipo.

Mimi, naridhia vigezo na masharti ya uanachama ya kifurushi cha

Saini

Tarehe

Siku	Mwezi	Mwaka
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

SEHEMU 7 - UPOKEAJI NA UHAKIKI WA FOMU (Kwa Matumizi ya Ofisi tu)

Ofisi ya Mkoa

Cheo

Jina la Afisa

Saini

Siku	Mwezi	Mwaka
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

Muhuri.....

Tarehe

Siku	Mwezi	Mwaka
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>